



WEKA SAUTI YAKO KWENYE WITO

MAFUNZO YA BIBLIA KWA VIKUNDI VIDOGO KATIKA USHIRIKA WA ANGLIKANA

MAELEZO KWA WAWEZESHAJI

Karibu

Nyenko hizi za Kujifunza Biblia zimeandaliwa kama sehemu ya Awamu ya 3 ya Lambeth Conference na Miito ya Lambeth. Kila somo la Biblia litafuata mada moja wapo kwenye Miito ya Lambeth. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti ya Lambeth Conference.

'Wito na Mwitikio' – Muundo wa Kujifunza Biblia

Kila moja kati ya Miito ya Lambeth hutolewa kwa Ushirika wa Anglikana – ikihitaji mwitikio. Somo la Biblia limejikita kwenye muundo wa 'Wito na Mwitikio', kulingana na hatua tatu:

1 - Sikia Wito

Wito wa Lambeth unachunguza nini na unamaanisha nini? Pokea msaada kutoka kwa sauti zenyenye maarifa kutoka kwenye Ushirika (ama kupitia kutazama video ya utangulizi au kupitia kusoma maelezo ya utangulizi).

2 - Sikiliza Maandiko

Nenda kwenye vifungu muhimu vinavyozungumzia mada ya Wito huu na usikilize jinsi vinavyoweza kuongoza mwitikio wako mwenywewe.

3 - Onyesha Mwitikio

Fanyeni kazi kwa pamoja na muamue jinsi mtakavyoweka katika vitendo mwitikio wenu kuhusu Wito.

Kujianaa kwa ajili ya kipindi chako:

- 1 Kabla ya kipindi toa nakala ya Wito wa Lambeth kwa kila mtu kusoma mbele ya mkutano. Unaweza kuipakua kutoka kwenye tovuti ya Lambeth Conference.
- 2 Kikundi kinapokutana, weka mazingira mazuri ili washiriki waweze kujisikia nyumbani na kusikilizana kwa uwazi na unyenyekevu.
- 3 Ongoza kwa maombi ya ufunguzi, ukimwalika Roho wa Mungu kufungua mioyo na akili ili kuelewa mawazo ya wengine.
- 4 Fanya utangulizi wa Wito wa Lambeth kuhusu Uanafunzi na waalike washiriki wa kikundi kushiriki mawazo na maswali yoyote ya awali.
- 5 Itazame video ya utangulizi mapema na uionyeshe wakati wa Somo la Biblia – pamoja na maelezo yoyote ya utangulizi.
- 6 Soma vifungu vya Biblia polepole na kwa maombi.
- 7 Maswali ya majadiliano yaliyochapishwa yanaweza kutumika kuhamasisha majadiliano au unaweza kuandaa mengine. Hakuna majibu sahihi au yasiyo sahihi.
- 8 Mwalike kila mshiriki kushiriki kile alichojifunza na jinsi mtazamo wake ulivyobadilika (au unavyobadilika).
- 9 Mhimize kila mshiriki aonyeshe mwitikio wa kiutekelezaji (madogo au makubwa) kwa kile alichojifunza, ili kuwekwa katika vitendo katika wiki ijayo.
- 10 Funga kwa ombi.

Kuunda sehemu salama na yenye kutia moyo

Inapendekezwa kwamba vikundi nya kujifunza viwe vidogo, vikiwa na watu sita au kumi, ili kuwe na fursa kwa kila mtu kuchangia.

Unapoweka mazingira salama kwa ajili ya mazungumzo na kujifunza kwa pamoja, wawezeshaji wanapaswa kufahamu mienendo ya ushawishi katika kikundi (kama vile rangi, jinsia, tabaka, umri, kiwango cha elimu, nk) Washiriki wanaweza kuwa na mitindo tofauti ya kujifunza au viwango tofauti nya maarifa kuhusu mada hiyo. Huenda wengine hawakuwa na fursa nyngi za kusikiliza sauti kutoka tamaduni nyngine.

Wawezeshaji wanapaswa kutia moyo, kuongoza na ustahimilivu. Weka fursa kwa ajili ya ujifunzaji binafsi, ukijua kwamba kila mshiriki anajifunza kwa njia na kasi yake mwenyewe.

Mbali na kuweka mazingira salama, ni muhimu kuzingatia muktadha na utamaduni wa eneo husika kwani hii inaathiri uzoefu wa washiriki. Kuingia kwenye mazungumzo na wengine kutatuonyesha kioo ambacho kitatumika kuangalia upya muktadha wa mwagine. Wawezeshaji wanaweza kubadilisha maswali kulingana na muktadha wa mahali husika na kuongeza maswali mengine.

Tarajia Roho Mtakatifu akuongoze upate ufahamu na uelewa mpya.

Simulia Hadithi Yako – Ujumbe kutoka kwa Askofu Jo

Katika kila awamu ya Safari, unaalikwa kushiriki jinsi Wito wa Lambeth ulivyo kwako katika muktadha wako. Unaweza kuchagua kushiriki sala, picha, ushuhuda mfupi au hadithi, maelezo kuhusu kuhusu moja ya miradi yako.

Tafadhalishiriki kuitia tovuti yetu:
<https://www.lambethconference.org/phase-3/share-your-story/>

Au wasiliana nasi kuitia mitandao ya kijamii:
Facebook: /LambethConference
Instagram: /LambethConference
Twitter: @LambethConf

Au barua pepe Askofu Jo Bailey Wells:
ShareYourStory@lambethconference.org

